Dodoma, 22 Februari, 2023

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI ZA TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA KWA KIPINDI CHA MIAKA MIWILI YA UONGOZI WA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

1.0. UTANGULIZI

Ndugu Waandishi wa Habari,

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai, kutujalia nguvu na afya ya kutekelekeza kwa ufanisi majukumu yetu ya kuwatumikia Watanzania.

Pili, napenda kuwashukuru ninyi Waandishi wa Habari na kuwapongeza kwa jinsi ambavyo mmeendelea kuelezea na kuwafikishia wananchi taarifa za kazi nzuri inayofanywa na Serikali yetu zinazohusu Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Tunaamini kuwa ninyi ni wadau muhimu katika mchakato wa maendeleo kwani kupitia kwenu, taarifa mbalimbali zinazohusu Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania zimekuwa zikiwafikia umma wa Watanzania na sehemu zingine nje ya Tanzania.

Leo nitaelezea utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana tangu nchini yetu ilipopata uhuru miaka 61 iliyopita, taarifa hii ya leo itajikita hasa katika kuelezea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ni Taasisi ya Serikali, iliyoundwa mwaka 2005 kwa Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura ya 346 ya Sheria za Tanzania. TCU ilitokana na maboresho yaliyofanywa na Serikali kwa lililokuwa Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu (HEAC) lililoanzishwa mwaka 1995 kwa Sheria ya Elimu Sura ya 523 ya Sheria za Tanzania.

Jengo la Wizara ya Elimu, Syansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam
Simu +255 22 2113694/ 2113691, Nukushi +255 22 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz

Lengo la kuanzishwa HEAC ilikuwa kuthibiti ubora wa vyuo vikuu nchini vilivyokuwa vinaanzishwa na kuendeshwa na taasisi binafsi. Uanzishwaji wa vyuo hivyo vinavyomilikiwa na taasisi binafsi ulitokana na mabadiliko yaliyofanywa na serikali katika uendeshaji wa elimu ya juu mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990. Mabadiliko haya ya mfumo yalitokana na kuridhiwa kwa sera huria katika utoaji wa elimu ya juu (liberisation of higher education). Ili kuweka mahusiano mazuri kati ya serikali na sekta binafsi (Public Private Partnership) na uoanishaji wa elimu itolewayo na vyuo vikuu nchini (*harmonisation of university education*), na kwa kuzingatia kuwa suala la ubora ni mtambuka linahusu taasisi zote zinazotoa elimu ziwe taasisi za serikali au taasisi binafsi, Baraza lilifanyiwa maboresho yaliyopelekea kuundwa kwa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) mwaka 2005, ambayo iliongezewa majukumu ikiwa ni pamoja na kuthibiti ubora wa elimu katika vyuo vikuu vinavyomilikiwa na kuendeshwa na Serikali.

TCU ina majukumu makubwa matatu: Kwanza, ni kusimamia sheria, kanuni na taratibu za uanzishaji na uendeshaji wa vyuo vikuu nchini. Pili, kusaidia na kutoa miongozo kwa vyuo vikuu kuhusu uthibiti wa ubora wa vyuo vikuu, njia mbalimbali za uendeshaji wa vyuo, kuandaa na kuratibu mafunzo mbalimbali kwa wahadhiri, waendashaji na viongozi wa vyuo vikuu nchini. Na jukumu la tatu ni kutoa ushauri kwa umma, vyuo vikuu, na serikali kupitia waziri mwenye dhamana ya elimu nchini kuhusiana na mabadiliko mbalimbali ya sayansi, teknolojia, sera na mwelekeo wa elimu ya chuo vikuu nchini na duniani kwa ujumla.

Dira ya TCU ni kuwa taasisi inayoongoza kikanda katika kusimamia ukuaji na maendeleo endelevu ya elimu ya chuo kikuu. Dira hii inatekelezwa kupitia dhamira ya TCU ya kuhakikisha uwepo wa mifumo endelevu ya elimu ya ngazi ya chuo kikuu ili kupata wahitimu wenye elimu, maarifa, ujuzi na uwezo wa kustahimili ushindani kitaifa, kikanda na kimataifa.

2.0. MAFANIKIO

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura ya 346 ya Sheria za Tanzania. Mafanikio haya ni kielelezo na uthibitisho wa jinsi serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilivyoiwezesha TCU kuweza kutekeleza vizuri majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni, miongozo na taratibu za uendeshaji wa vyuo vikuu hapa nchini, kikanda na kimataifa. Baadhi ya mafanikio hayo ni yafuatayo:

2.1. Kuimarika kwa mifumo ya uthibiti ubora, ushauri na usimamizi wa elimu inayotolewa na Vyuo Vikuu hapa nchini

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania imeendelea kuimarisha mifumo yake ya uthibiti ubora na mifumo ya ndani ya vyuo vikuu ili kuhakikisha vyuo vikuu vinaendana na mwelekeo wa nchi, ambapo Tanzania imelenga kuwa Taifa la watu wenye maarifa, ujuzi, weledi na uwezo wa kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi kwa manufaa ya wananchi wake ifikapo mwaka 2025 pamoja na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati unaochochewa na uwepo wa viwanda.

Jengo la Wizara ya Elimu, Syansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam
Simu +255 22 2113694/ 2113691, Nukushi +255 22 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz

Katika kuhakiki ubora, TCU imeimarisha mifumo yake ya ushauri na ukaguzi wa mara kwa mara, wa kawaida na wa kushtukiza kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo kwa lengo la kuhakikisha kuwa elimu itolewayo na vyuo vikuu hapa nchini inakidhi viwango vya ubora kitaifa, kikanda, na kimataifa. Kwa mfano, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Februari, 2023 vyuo vikuu vyote 47 vilivyopo vimekaguliwa na kupewa ushauri wa maeneo yanayohitaji kuboreshwa. Zoezi hili la ukaguzi wa vyuo ni endelevu kila mwaka. Vilevile TCU imeweka utaratibu wa kuanzishwa na kuimarishwa mifumo ya uthibiti ubora ndani ya vyuo vikuu ambapo vyuo vyenyewe vimekua na utaratibu wa kujikagua, kujitathmini na kufanya marekebisho mbalimbali kwa kuzingatia miongozo ya uendeshaji wa vyuo vikuu.

Kimsingi, mifumo ya ushauri, ukaguzi, na ufuatiliaji wa mara kwa mara imefanya vyuo kufanya maboresho makubwa katika miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maabara za kisasa, mifumo ya mawasiliano ya kielektroniki, madarasa na kuongeza idadi ya viongozi na wahadhiri wenye sifa stahiki kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo.

2.2. Kuwajengea uwezo wahadhiri na viongozi wa vyuo vikuu kuhusiana na utolewaji wa elimu ya chuo kikuu

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania imeendelea kuandaa na kuratibu mafunzo kwa viongozi, wahadhiri na maofisa wa vyuo vikuu vya umma na binafsi hapa nchini kwa lengo la kuwajengea uwezo katika usimamizi na uendeshaji wa taasisi zao.

Kwa mfano, kuanzia mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 6.4 kupitia mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (*Higher Education for Economic Transformation-HEET)* kwa ajili ya kuimarisha uthibiti ubora na uhuishaji wa mitaala ya vyuo vikuu ambapo zaidi ya mitaala 300 ya vyuo vikuu iko katika hatua mbalimbali za kufanyiwa mapitio ili kuhuishwa kwa kuzingatia maoni ya wadau mbalimbali ili kukidhi matarajio yao na mahitaji ya soko.

Katika kufanikisha hili, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, imeendelea kuandaa na kuratibu mafunzo ya kubadilishana uzoefu kwa viongozi na wanataaluma wa vyuo vikuu kuhusiana na uendeshaji wa vyuo vikuu, utengenezaji mitaala inayozingatia ujuzi na inayoendana na soko, mbinu za ufundishaji kwa wahadhiri ambao hawakusoma fani za ualimu, ulinganifu wa programu za masomo (*programme benchmarks*), uthibiti ubora, na utengenezaji na utumiaji wa mifumo ya kompyuta. Kwa mfano, katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2022 jumla ya viongozi na wanataaluma 575 wameshanufaika na mafunzo hayo. Mafunzo hayo yamelipiwa na serikali kwa asilimia 100.

Kutokana na hatua hizi zinazochukuliwa na Serikali, vyuo vikuu vimeweza kuimarisha mifumo yake ya uthibithi ubora na uendeshaji wa mafunzo.

2.3. Kuongezeka kwa fursa za masomo ya elimu ya juu na idadi ya wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu nchini

Serikali imeendelea kutekeleza kwa vitendo azma yake ya kuongeza wigo wa fursa za masomo ya elimu ya juu kwa watanzania. Kwa mfano katika kipindi cha miaka miwili fursa mbalimbali za masomo zimeongezeka kama ifutavyo:

Jengo la Wizara ya Elimu, Syansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam
Simu +255 22 2113694/ 2113691, Nukushi +255 22 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz

i) Nafasi za masomo katika vyuo vya elimu ya juu katika programu za Shahada ya Kwanza zimeongezeka kutoka 157,770 mwaka 2020/21 hadi 172,168 mwaka 2022/23. Hili ni ongezeko la nafasi 14,398 sawa na asilimia 9.1.

ii) Programu za masomo ambazo zimeruhusiwa kudahili wanafunzi wa shahada ya kwanza zimeongezeka kutoka 686 mwaka 2020/21 hadi 757 mwaka 2022/2023.

iii) Wanaodahiliwa katika shahada ya kwanza wameongezeka kutoka 87,934 mwaka 2020/21 hadi 113,383 mwaka 2022/23 sawa na asilimia 28.9.

iv) Idadi ya Wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu imeongezeka kutoka 259,266 mwaka 2020/21 hadi 295,919 mwaka 2021/22 sawa na asilimia 14.1. Idadi hii inatarajiwa kuongezeka kwa mwaka wa masomo 2022/2023.

2.4. Kurahisishwa na kuimarishwa kwa utoaji wa huduma za udahili, na utambuzi wa tuzo zitolewazo na vyuo vikuu

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania imeimarisha mifumo yake ya kielektroniki inayotumika katika utoaji wa huduma mbalimbali kwa wadau mbalimbali wa elimu. Baadhi ya mifumo hiyo ni pamoja na mfumo wa pamoja wa kielekroniki kwa ajili ya kuratibu udahili wa shahada za kwanza kwa vyuo vyote vya elimu ya juu hapa nchini; Mfumo wa Utambuzi wa Tuzo za Wahitimu kutoka Vyuo Vikuu vya nje ya Tanzania; na Mfumo wa kuchakata maombi ya Hati ya Kutokuwa na Pingamizi kwa wananchi wanaotaka kwenda kusoma vyuo vikuu nje ya nchi.

Maboresho haya ya mifumo yameongeza tija na ufanisi na kurahisisha utoaji wa huduma kwa kuwawezesha wananchi na wadau mbalimbali kupata huduma bora na kwa haraka. Kwa mfano, muda wa uhakiki na utambuzi wa tuzo za nje ya nchi umepungua kutoka siku 14 za awali hadi siku tatu (03). Pia waombaji wa udahili wanaweza kutuma maombi yao moja kwa moja kwenye vyuo husika na kuthibitisha vyuo wanavyopenda popote walipo bila kulazimika kusafiri kwenda chuoni.

Aidha, kutokana ma maboresho ya mifumo hii, taarifa mbalimbali zinazohusu elimu ya juu hapa nchini sasa zinapatikana kwa urahisi kwa ajili ya matumizi ya taasisi mbalimbali za umma na binafsi. Kwa mfano, mfumo wa pamoja wa kielekroniki kwa ajili ya kuratibu udahili wa shahada za kwanza umeunganishwa na mfumo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar (ZHELB) na hivyo kurahisisha upatikanaji wa taarifa za udahili wa wanafunzi wa elimu ya juu ambao ni wanufaika wa mkopo na kuharakisha utoaji wa mikopo ya wanafunzi husika. Mifumo hii pia imewezesha kupatikana kwa taarifa na takwimu mbalimbali zinahusiana na vyuo vikuu hapa nchini kama vile idadi ya wanafunzi, wahitimu, wahadhiri, viongozi, wafanyakazi waendeshaji, mitaala, n.k., hivyo kurahisisha mipango ya serikali na wadau mbalimbali wa elimu ya juu hapa nchini. Hivyo, licha ya vyuo vikuu, wadau wengine ambao hadi sasa wamenufaika kutokana mifumo yao kuunganishwa na TCU ili kujipatia taarifa mbalimbali ni pamoja na Wizara ya Afya, na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Jengo la Wizara ya Elimu, Syansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam
Simu +255 22 2113694/ 2113691, Nukushi +255 22 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz

2.5. Kuimarishwa kwa programu za Elimu kwa Umma kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Elimu ya Chuo Kikuu

Tume imeimarisha mifumo yake ya utoaji wa elimu kwa umma na hivyo kuweza kuwafikia wadau wengi zaidi. Elimu kwa umma imekuwa ikitolewa kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

i) Kutembelea wahitimu wa kidato cha sita waliopo kwenye mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa nchi nzima na kufanya mikutano nao kwa lengo la kuwaelimisha kuhusu taratibu za udahili. Kwa mfano kwa mwaka 2022/23 elimu kwa umma imetolewa katika jumla ya Kambi 20 za Jeshi la Kujenga Taifa ambapo jumla ya wahitimu 25,144 wa Kidato cha Sita walifikiwa.

ii) Kuandaa Maonesho ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ambayo hufanyika kila mwaka. Maonesho haya yameendelea kuboreshwa katika kipindi hiki na hivyo kuvutia taasisi nyingi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki katika kuonesha huduma na bidhaa zao. Kwa mfano, idadi ya taasisi zinazoshiriki maonesho imeongezeka kutoka 67 mwaka 2020/21 hadi 78 mwaka 2022/23. Aidha, idadi ya wananchi wanaotembelea maonesho haya imendeelea kuongezeka hasa kutokana na baadhi ya vyuo vya elimu ya juu kuanza kutoa huduma ya udahili wakati wa maonesho.

iii) Kuendelea kushiriki katika Maonesho ya Wiki ya Elimu ya Juu Zanzibar ambayo hufanyika kila mwaka. Mfano katika maonesho ya mwaka 2022 zaidi ya wananchi 8,321 wakiwemo wahitimu wa Kidato cha Sita walifikiwa na kupewa elimu kuhusiana na masuala yanayohusu utolewaji wa elimu ya chuo kikuu nchini Tanzania na nje ya Tanzania.

Kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu majukumu ya TCU na taratibu za uendeshaji wa elimu ya chuo kikuu kumepunguza kwa kiasi kikubwa changamoto wanazokutana nazo wanafunzi na wadau wengine wa elimu ya juu katika kipindi hiki ikilinganishwa na miaka iliyopita. Aidha, wanafunzi wameendelea kuwa na utulivu katika kufuatilia masomo yao na kuwasilisha maoni yao au malalamiko yao katika mamlaka husika kwa urahisi na kuwa na majadiliano na mtazamo chanya katika kutafuta suluhu kila changamoto zinapojitokeza.

3.0. HITIMISHO

TCU inawashukuru wadau mbalimbali wa elimu ya chuo kikuu kwa ushirikiano wanaotoa ikiwamo Serikali, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Vyuo Vikuu, Wanafunzi, Wazazi, Bodi za Usajili wa Wataalamu, Waajiri, Bodi za Mikopo za Bara na Zanzibar, na wadau wote kwa ujumla wa ndani na nje ya Tanzania.

Imetolewa na:

Prof. Charles D. Kihampa
KATIBU MTENDAJI
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA

Jengo la Wizara ya Elimu, Syansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam
Simu +255 22 2113694/ 2113691, Nukushi +255 22 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz